Sifa za Watu Binafasi na Mashirika ya Korea Kaskazini Yaliyoorodheshwa

1.1 UTANGULIZI

Ili kufanya juhudi ya kupunguza na mbeleni kukomesha shughuli ambazo si za usambazaji zinazofanywa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea (DPRK), Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) limeidhinisha vikwazo vinavyolenga watu binafsi na mashirika maalum (walioorodheshwa) wanaoaminiwa kuwa, au wanaofanya aina hizi za ukiukaji huku wakijua wanayoyafanya. Nchi wanachama za Umoja wa Mataifa na mashirika yanayojumuishwa kwenye mamlaka yao (k.v., biashara, mawakala ya serikali, raia, n.k.) yanatarajiwa kutekeleza kisheria vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Hata hivyo, maelezo ya kutambua na kufuatilia shughuli za walioorodheshwa mara nyingi huwa ni kidogo au ni taabu kuipata. Ili kusaidia kukuza uwezo wa nchi kutekeleza vikwazo vya Baraza la Usalama dhidi ya wakiukaji wa Korea Kaskazini, ni muhimu kujua sifa za pamoja za shughuli na ukiukaji wa kanuni, zinazoshirikiwa na vikundi hivi kama mbinu ya ziada ya kubainisha wakiukaji hawa au wakiukaji wengine wa vikwazo wawezekanao. Uchunguzi huu wa kitafiti unakagua sifa za pamoja za watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa kwenye mfumo wa Korea Kaskazini, na unatoa mapendekezo yanayoweza kuidhinishwa na mataifa na wahusika wengine husika kuhusiana na wakiukaji hawa na wakiukaji wengine wawezekanao.

1.2 MUHTASARI WA MBINU

Tathmini ya watu binafsi na mashirika yote (k.v., kampuni, mashirika, mawakala, n.k.) yaliyoorodheshwa kwenye mfumo wa vikwazo vilivyowekewa Korea Kaskazini ilifanywa ili kuchunguza sababu za kuorodheshwa, ukiukaji uliofanywa, maelezo ya kuunga mkono ikiwa yapo, na nadharia zozote ambazo zingeweza kufanywa pasipokuwepo maelezo ya ziada.[1] Kila ukiukaji ulipewa alama kulingana na ubora wa maelezo

[1] Rejelea orodha ya watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa kwenye mfumo wa Korea Kaskazini (zilizoorodheshwa kama KPi na KPe kwenye hati) hapa:

Rico Carisch
rico.carisch@comcapint.com
+1-610-390-9541

www.comcapint.com
110 West 94 Street – 2D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
loraine.rickard-martin@comcapint.com
+1-917-715-2142

unaouunga mkono, huku alama kubwa zikipewa maelezo ya Umoja wa Mataifa na maelezo ya kutoka nje ambayo yanaaminika (k.v., ripoti za kuaminika za vyombo vya habari). Data hii kisha ilichambuliwa ili kupata ruwaza, kama vile ukiukaji unaofanyika mara kwa mara, sifa za pamoja, maelezo madhubuti na dhaifu, n.k., na pia mazingatio ya kipekee au yanayoweza kuwa muhimu. Matokeo kwenye utafiti huu wa kifani yanatoka kwenye data iliyochukuliwa kuwa maelezo muhimu kuhusu ukiukaji kulingana na ripoti za Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ambayo inamaanisha kuwa ruwaza zilizoripotiwa ni za kuaminika sana.

1.3 MATOKEO

Kuna sifa kadhaa za pamoja, zenye nguvu au zilizo dhaifu, zinazoshirikiwa na watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa yawekewe vikwazo vya Umoja wa Mataifa. Maelezo machache yanajulikana kuhusu watu binafsi walioorodheshwa na mashirika yaliyoorodheshwa; licha ya hayo, vikundi hivyo mara nyingi huwa vina uhusiano anuwai rasmi au usio rasmu (k.v., waajiriwa wa mashirikisho, kuwepo kwa usimamizi wa serikali kwenye mashirika fulani, maingiliano ya kidiploamasia, au kupitia mawakala na vitengo vya kijeshi) na kutokana na haya, baadhi ya sifa kuhusu mashirika zinaweza kupanuliwa zihusishe watu binafsi.

1.3.1 WATU BINAFSI

Jopo la Wataalamu la Korea Kaskazini na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa zimetoa maelezo machache sana kuhusu kwa nini watu mahususi wamelengwa na vikwazo, lakini baadhi ya sifa zipo. Sifa ya pamoja zaidi inayoshirikiwa na karibu watu watu wote walioorodheshwa ni kuwa wanafanyia kazi shirika lililoorodheshwa. Kati ya watu 80 walioorodheshwa, hakuna sababu maalum iliyotolewa ili kuelezea vikwazo dhidi ya watu 57 isipokuwa ilikuwa wanalifanyia kazi shirika lililoorodheshwa. Watu walioorodheshwa hasa huwa wanafanya kazi kwenye benki au kampuni za biashara (46), ambazo zinafuatwa na mawakala ya silaha, ndege, au nyuklia (16), na kisha kuna mawakala ya serikali ya daraja za juu (12, k.v., chama cha utawala, wakala ya ujasusi (tazama Jedwali la 1). Watu wachache wanawakilisha mawakala ya serikali ya Korea Kaskazini kwenye nchi zingine, na wana hadhi ya kidiplomaisa au wanashukiwa kuwa ni maafisa wa ujasusi (4).

Kutokana na tathmini, aina za nyadhifa zinazoshikiliwa na watu walioorodheshwa wanaofanya shughuli nchini Korea Kaskazini mara nyingi huwa ni maafisa wakuu kama vile wakurugenzi, rais wa kampuni, au mawaziri wa serikali. Kila moja kati ya sekta hizi tatu nchini Korea Kaskazini huwa zinawekewa vikwazo kwa kiwango sawia, baina ya

---

https://www.un.org/securitycouncil/content/un-sc-consolidated-list. Maumbizo anuwai yanapatikana.

watu 12 na 14 kutoka kwenye kila sekta (Jedwali la 1). Hata hivyo, hii ni tofauti sana tunapochunguza vikwazo vilivyowekewa watu binafsi wanaofanya shughuli nje ya Korea Kaskazini. Isipokuwa wanadiplomasia wanne waliowekewa vikwazo, watu 32 waliowekewa vikwazo walikuwa wanafanya kazi kwenye benki au kampuni za biashara. Idadi kubwa ya watu hawa wanafafanuliwa kama wawakilishi wa ng'ambo, wachache ambao wanafafanuliwa kama Mwakilishi Mkuu. Ili kufanya shughuli kwa niaba ya waajiri wao, walioorodheshwa wanakiuka katazo la usafiri.

Jedwali la 1: Aina ya shirika inayoajiri walioorodheshwa ndani na nje ya Korea Kaskazini

	Mtu binafsi ambaye hasa anafanya kazi ndani ya Korea Kaskazini	**Mtu binafsi ambaye hasa anafanya kazi nje ya Korea Kaskazini**
Benki na kampuni za biashara	14	32 (1 amejifanya ni mwanadiplomasia)
Mawakala ya silaha, ndege, au nyuklia	14	2 (wanadiplomasia, wote Siria)
Mawakala ya serikali ya daraja za juu	12	2 (wanadiplomasia, Misri na Burma)

Watu walioorodheshwa wanaofanya kazi nje ya Korea Kaskazini mara nyingi huwa wanafanya shughuli zao nchini Uchina na Siria, na kwenye maeneo ya Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati (tazama Jedwali la 2). Uchina ni sehemu murwa ya shughuli za Korea Kaskazini kwa ajili iko karibu sana nayo, kwa ajili ya uchumi wake mkubwa, imara, na kwa ajili ya uhusiano wake mzuri kiasi na Korea Kaskazini. Watu wote walioorodheshwa wanaofanya shughuli nchini Uchina wanafanya kazi kwenye kampuni za biashara au taasisi za benki,[2] na ukiukaji unaofanywa na mashirika haya unajumuisha biashara ya bidhaa za usambazaji, ufadhili wa shughuli za usambazaji, na ufadhili wa mashirika mengine yaliyowekewa vikwazo yanayofanya biashara ya bidhaa za usambazaji. Watu kadhaa walioorodheshwa wanaofanya shughuli nchini Uchina ni wawakilishi wa Benki ya Biashara ya Nje ya Korea Kaskazini, shirika linaloendeshwa na serikali.[3] Kutokuwepo wawakilishi kutoka Shirika la Biashara za Kuendeleza Uchimbaji Madini la Korea (KOMID) wanaofanya shughuli nchini Uchina kunashangaza. KOMID ilikuwa inajulikana kama wauzaji nje/waingizaji nchini Korea Kaskazini wa silaha za kawaida, nyenzo za usambazaji zinazohusu makombora ya mbali, na wakandarasi wa jumla wa miradi ya ujenzi wa kijeshi na kiraia. Kwa mujibu wa shirika moja pekee, wengi kati ya walioorodheshwa wanaofanya shughuli zao nje Korea Kaskazini waliifanyia kazi KOMID.[4]

---

[2] Watu binafsi walioorodheshwa wa 57, 59, 62, 64, 68, 72, na 77.

[3] Benki ya Biashara ya Nje, tazama S/2018/171, paragrafu za 162-165.

[4] Watu walioorodheshwa wanaofanya kazi na KOMID ambao wanafanya shughuli nchini Korea Kaskazini wanajumuisha wa 10, 11, na 22; huku walioorodheshwa wanaofanya kazi na KOMID ambao wanafanya shughuli nje ya Korea Kaskazini wanajumuisha wa 17, 20, 24, 27, 30, 31, 33,

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Jedwali la 2: Wananchi walioorodheshwa wanafanya shughuli kwenye kampuni wanazowakilisha

	Watu binafsi ambao hasa wanafanya kazi ndani ya Korea Kaskazini	Watu binafsi ambao hasa wanafanya kazi nje ya Korea Kaskazini
Watu wanaofanya kazi nchini:		
Uchina		7
Siria		5 (2 ni wanadiplomasia)
Sudani		3
Vietinamu		3
Irani		2
Urusi		2
Misri		1 (mwanadiplomasia)
Libya		1
Bama		1 (mwanadiplomasia)
Malesia		1
Kuba		1
Nchi kadhaa		10
Watu walioajiriwa na:		
KOMID	3	10
Benki ya Biashara ya Nje	1	7
Benki ya Kibiashara ya Tanchon	5	5
Taasisi zingine za benki na biashara	4	13

Badili yake, walioorodheshwa wanaofanyia kazi KOMID nje ya Korea Kaskazini wanafanya shughuli kwenye nchi zisizokuwa imara zikiwemo Siria, Irani, Sudani, na Bama. Siria inazusha wasiwasi kwa muktadha huu. Watu hawa walioorodheshwa huwa wanawekewa vikwazo hasa kwa kufanya biashara haramu ya bidhaa za usambazaji kama vile vijenzi vya makombora ya mbali (k.v., bidhaa zinazoweza kutumiwa kuunda makombora ya Skadi ya Siria)[5], huku mtu mmoja aliorodheshwa kwa kufanya miamala ya fedha (benki) inayohusu biashara ya silaha[6]. Walioorodheshwa wanaofanya biashara ya bidhaa haramu wanafanyia kazi KOMID au ni wanadiplomasia wa Wizara ya Usalama wa Nchi ya Korea Kaskazini wanaofanya biashara kwa niaba ya KOMID.

Mbali na Siria na mataifa mengine yaliyoorodheshwa kwenye Jedwali la 2, mataifa kadhaa mengine ya Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati ni maeneo muhimu ya shughuli za watu binafsi walioorodheshwa. Tunisia, Libya, Saudia, Muungano wa Falme za Kiarabu, na mataifa mengine ni maeneo yanayozuriwa mara kwa mara na watu

34, 36, na 56.

[5] Tazama S/2017/150, Jedwali la 8 kwenye paragrafu ya 206; S/2017/742, paragrafu ya 28; S/2017/742, paragrafu ya 29).

[6] Mtu binafsi aliyeorodheshwa wa 16.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

binafsi kama sehemu ya mpito au ili kufanya miamala kwa niaba ya mashirika yaliyoorodheshwa.[7]

Zingatio moja la kipekee linalovuta makini ni kutumia vituo vya kidiplomasia ili kukwepa vikwazo. Kwenye mfano wa shirika la #1, KOMID mara nyingine ilituma nyaraka za usafirishaji (zinazofafanua yaliyomo kwenye bidhaa zinazosafirishwa ili zipitishwe mipakani) kupitia pochi la kidiplomasia hadi kwenye balozi zilizoko kwenye mataifa mengine. Hii inapinga ukaguzi mipakani kwa njia mbili. Inasababisha ukawiaji mrefu mpaka nyaraka mwafaka zipatikane kwa sababu mapochi ya kidiplomasia hayawezi kufunguliwa, na inayazuia mawakala ya mipaka yasiweze kukagua yaliyomo kwenye kontena za usafirishaji zinapowasili kwa sababu nyaraka zilitumwa kupitia njia nyingine.

Ili kukwepa vikwazo, watu kadhaa walioorodheshwa walibadilisha mfuatano wa herufi wa majina yao au walitumia lakabu. [8] Ingawa ingeweza kuchukuliwa kuwa watu wengi au wote wanaofanya shughuli nje ya Korea Kaskazini wanabadilisha majina yao au nyaraka zao za usafiri, baadhi ya mabadiliko ya mfuatano wa herufi yanaweza kusababishwa na tofauti za ufasiri baina ya vibambo vya Korea na vile vya lugha zingine.[9]

1.3.2 MASHIRIKA

Kwa kulinganisha na watu binafsi, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limetoa maelezo zaidi kuhusu ukiukaji uliofanywa na mashirika 75 ya Korea Kaskazini yaliyoorodheshwa. Mashirika haya yanaweza kuwa yameorodheshwa kwa ajili ya takriban aina 30 tofauti za ukiukaji. Zinatofautiana kuanzia ukiukaji wa kipekee sana unaolenga watawala maalum, kama vile kutumia uuzaji wa bidhaa za anasa ili kufadhili shughuli za usambazaji, hadi ukiukaji ambao mara nyingi unaonekana kwenye mifumo anuwai ya vikwazo kama vile uuzaji na ununuzi wa silaha zilizowekewa marufuku.

Kama vile watu binafsi walioorodheshwa, ukiukaji mwingi unaofanywa na mashirika yaliyoorodheshwa unahusu kufanya kazi na au kuwa sehemu ya shirika lingine lililiooroidheshwa. Hii huenda isishangaze kwa ajili mashirika mengi yameunda kampuni zifichazo, yamebadilisha mfuatano wa herufi za majina yao, au yamebadilisha majina yao ya kufanyia shughuli kama mbinu ya kukwepa vikwazo. Kutumia lakabu ni shughuli ya pili inayotumika sana inaayoonekana kwenye mashirika yaliyoorodheshwa na Umoja wa Mataifa. Kwa mfani, kampuni kadhaa zilizoorodheshwa za biashara na benki (k.v., mashirika ya 14, 15, 17, 24, 25, na mengine) zinatumia lakabu ya, ni kampuni

[7] Kwa mfano, tazama S/2018/171, Nyongeza ya 43 na paragrafu za 162-168.

[8] Kwa mfano walioorodheshwa wa 16, 18, 19, 20, 25, 30, 74, na 80 wote wanachukuliwa kuwa wanatumia lakabu au hati bandia ili kukwepa kugunduliwa.

[9] Kwa mfano, hii ndiyo inaweza kuwa hali kuhusiana na waliorodheshwa wa 51, 70, na 75.

zinazomilikiwa na, au zinamilikiwa na shirika la kwanza lililoorodheshwa, KOMID. Licha ya hayo, kwa takriban robo ya mashirika yaliyoorodheshwa, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa halijatoa ithibati yoyote kuwa ymefanya ukiukaji wowote mbali na kufanya kazi na shirika lililoorodheshwa.

Kuhusiana na vikwazo vya fedha vya Umoja wa Mataifa, ukiukaji unaotumika sana ni ule unaofanywa na mashirika yanayorahisisha ukiukaji wa ukwamishaji mali ya mashirika mengine yaliyoorodheshwa.[10] Mengi kati ya mashirika haya pia yanarahisisha uhamishaji fedha ili kurahisisha ukiukaji wa vikwazo. Mengi kati ya mashirika haya yamepatikana kuwa yanatumia Jumuiya Mawasiliano Anga ya Fedha Baina ya Banki Ulimwenguni (SWIFT), mtandao murwa wa kurahisisha malipo baina ya benki unaotumiwa na kumilikiwa na benki kuu ulimwenguni.[11] Pindi yanapogunduliwa, mashirika huwa yanajitoa kwenye SWIFT au SWIFT inayapinga yasiweze kuufikia mfumo na inafunga akaunti zao.[12]

Tunapozungumzia marufuku, miongoni mwa takriban thuluthi tatu za mashirika ambayo Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limetoa ithibati madhubuti ya ukiukaji, mashirika mengi huwa yamewekewa vikwazo kwa ajili ya mojawapo kati ya mbinu tatu za ukiukaji: kufanya biashara ya bidhaa zilizowekewa marufuku, kufanya biashara au kurahisisha biashara ya nyenzo zilizowekewa marufuku, na kusimamia, au kuhusika kwenye, uundaji wa silaha za maangamizi makubwa (WMD). Mashirika yanayofanya biashara ya bidhaa zilizowekewa marufuku, karibu zote huwa ni kampuni za usafirishaji na mara nyingi zinatumia mbinu halisi za ulaghai, kama vile kubadilisha au kufunika majina ya vyombo vya usafiri, kama mbinu ya kukwepa vikwazo.[13] Bidha zinazotajwa sana kuwa zinafanyiwa biashara ni petroli/mafuta na makaa. Mashirika haya pia yanaashiria kuwa usafirishaji wao unaelekea Vietinamu au Urusi, lakini pia Singapoo na Uchina (ingawa baadhi ya meli hazikufika kwenye vituo vyao vya mwisho vya usafiri). Wakati wa kuandika haya, mashirika yanayofanya ukiukaji hayaonekani kuwa yameorodheshwa kwa ukiukaji wa vikwazo vyovyote vingine. Meli nyingi ni vyombo vyenye bendera ya Korea Kaskazini, na zile zenye bendera ya nchi zingine mara nyingi huwa zinatoka kwenye eneo la Karibiani, haswa Panama.[14]

---

[10] Kwa mfano, tazama mashirika ya 14, 17, 23, au 33.

[11] SWIFT haihamishi fedha halisi, lakini inaruhusu benki zipeane maelezo ya uhamisho wakati wa kuhamisha fedha. Mfumo wa msimbo unaotumiwa kwenye ujumbe wa SWIFT unatoa maelezo kuhusu benki, mji, nchi na jina la mtu mtu binafsi au shirika linalopokea fedha.

[12] Kwa mfano, tazama mashirika 23, 33, 35, 45, 47, au 49.

[13] Tazama walioorodheshwa wa 10 na kikundi cha hizvi karibuni zaidi cha walioorodheshwa, nambari 55 hadi 75.

[14] Mashirika ya 55, 64, na 67 yalikuwa na bendera ya Panama, shirika la 73 lilikuwa na bendera ya St. Kitts-Nevis, shirika la 75 lilikuwa na bendera ya Jamhuri ya Dominika, na shirika la 61 lilikuwa na bendera ya Siera Leoni.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Mashirika yaliyowekewa vikwazo kwa ajili ya kufanya biashara au kurahisisha biashara ya nyenzo zilizowekewa marufuku yana uwezekano mkubwa zaidi kuwa yanafanya aina zingine kadhaa za ukiukaji.[15] Nyingi kati ya ukiukaji huu zinaonekana kuwa zinajumuisha niashara ya silaha na nyenzo za usambazaji, lakini mashirika machache kati ya haya pia yameonyeshwa kuwa yamehusika moja kwa moja na uundaji wa nyenzo za usambazaji.[16] Mashirika haya ni mchanganyiko wa mawakala ya benki, biashara na serikali. Mwishowe, watu walioorodheshwa waliofanya, au waliohusika kwenye uundaji wa Silaha za Maangamizi Makubwa mara nyingi huwa ni mawakala ya serikali ya Korea Kaskazini tu, kama vile Usimamizi wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Vyombo vya Anga au Chuo cha Pili cha Sayansi.[17]

1.4 MAHOJIANO NA MAPENDEKEZO

Kutokana na tathmini ya watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ruwaza fulani za sifa za wakiukaji zinaweza kuonekana na zinaweza kuwa muhimu kwa nchi zinazotaka kuvitekeleza vizuri zaidi vikwazo.

Miongoni mwa watu binafsi, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limetaja wazi kuwa wale wanaofanyia kazi mashirika yaliyoorodheshwa pia wataorodheshwa. Kwa nchi zinazotaka kutekeleza sheria za vikwazo au kufichua ukiukaji, itakuwa muhimu kufuatilia shughuli za watu muhimu, haswa wale wenye wadhifa wa uongozi au wale wanaosafiri au kufanya biashara kwa niaba ya shirika lililoorodheshwa.

1. Shughuli za watu binafsi walioorodheshwa zinaonekana kuwa ni muhimu haswa kwenye nchi na maeneo fulani. Kama nchi ya karibi iliyo na nguvu kubwa kifedha, Uchina inaonekana kuwa ni kituo muhimu kwa shughuli za kifedha za watu binafsi walioorodheshwa. Kwa ziada, kuwa hakuna walioorodheshwa wanaofanyia kazi KOMID, kampuni kuu ya biashara ya silaha inayoendeshwa na serikali, wanaofanya shughuli zao nchini Uchina inadokeza kuwa shughuli kuu ya Uchina ni kutumika kama eneo la biashara ya kifedha na labda nchi ya ambapo Korea Kaskazini inapata teknolojia nyeti, na uwezekano ni mdogo kuwa Uchina ni kituo cha biashara za kijeshi za moja kwa moja. Hii inaonekana kuwa inaungwa mkono kwa kuzingatia kuwa Siria na mataifa mengine yasiyokuwa na amani ndiyo maeneo makuu ya shughuli kwa shughuli zote za KOMID na shughuli zingine za usamabazaji za Korea Kaskazini. Inaonekana kuwa Korea Kaskazini inawatumia kwa mpango wawakilishi wa KOMID ili kutekeleza biashara ya silaha kwenye mataifa yasiyokuwa na amani.

[15] Kwa mfano, tazama mashirika ya 1, 4, 7, 10, 14, 17, 18,

[16] Kwa mfano, tazama walioorodheshwa wa 1, 7, 18, 21, na 44

[17] Tazama walioorodheshwa wa 1, 7, 12, 16, 18, 21, 27, 28, 29, 39, 44, na 46.

Ili kutekeleza upya kisheria vikwazo vya Umoja wa Mataifa, nchi wanachama zinafaa kuupati kipaumbele ufuatilizi wa biashara ya silaha kwenye maeneo yasiyokodhesha wa zinafaa kufuatiliwa na vita, haswa kufuatiliwa wawakilishi wa KOMID na mashirikishoi mengine ya serikali ya Korea Kaskazini, na kuupatia kipaumbele ufuatilizi wa biashara ya fedha kwenye maeneo tuliyu zaidi, ili kuwasaidia wanachama wa Umoja wa Mataifa waweze kutumia rasilimali zao kwa ufanisi zaidi.

2. Kwenye maeneo, shughuli za watu binafsi walioorodheshwa zinafaa kufuatiliwa kwenye mataifa anuwai kwenye Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati. Maeneo haya ima ni vituo vya mpito au sehemu za kufanyia biashara ya silaha kwa nchii kadhaa ikiwemo Korea Kaskazini. Inawezekana kuwa nchi hizi hazina uwezo wala ari ya kisiasa ya kufuatilia shughuli za watu hawa. Nchi zenye vita, au zile zenye serilali dhaifu, zinaonekana kuwa ni makao makuu ya shughuli za Korea Kaskazini. Kimahususi, Siria, na kwa kiwango kidogo Sudani na Irani, zinaonekana kuwa ni nchi zinazopendelewa na Korea Kaskazini na zinaokana kuwa ni sehemu muhimu za biashara yake ya silaha.

Shughuli za Korea Kaskazini, kimahususi zinazofanywa na KOMID, mashirikisho mengine y Korea Kaskazini, au wawakilishi wa Usaama wa Nchi ya Korea Kaskazini, zinawekuwa mjaa ya fedha, zinafaa kufuatiliwa kwenye nchi zenye vita.

3. Matumizi ya lakabu na kubadilishi ya majina inaonekana kuwa mjaa ya fedha ya ukwepaji kwa watu walioorodheshwa wa Korea Kaskazini, haswa yanapofasiriwa hadi lugha zingine kama vile Kiingereza. Kwa kuzingiatia kuwa baadhi ya walioorodheshwa wanajulikana kuwa wanatumia lakabi au hati bandia, inaweza kuwa muhimu kuwapatia maafisa wa mipaka na mpito orodha ya lakabu, na pia michangayiko ya herufi za jina inayoweekana. Pale kuna programu ya kuchanganua majina, inaweza kuwa muhimu kuhusisha mfuatano mbadala wa herufi za mjina kama sehemu ya programu ya utafutaji. Hata hivyo, tahadhari inaeleweka kwa ajili vigezo vengine vya watu hawa vinafaa kupatikana kwenye maeneo ya mpito (k.v., mwajiri wa aliyeorodheshwa) ili kuhakikisha kuwa makosa hayafanywi kuhusiana na watu binafsi ambao hawajaorodheshwa.

Nchi wanachama inaweza kuboresha ufanisi na utenda kazi wa ufuatilizi wa watu binafsi walioorodheshwa kwa kuwapatia mawakala yao ya mipaka orodha za, programu zenye, majina watu binafsi walioorodheshwa, mfuatano kimakosa wa herufi za jina unaotokea mara kwa mara, na maelezo ya ziada ya kutambulisha.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin
Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142
Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

4. Kuhusiana na mashirika, kama vile watu binafsi, mashirika kimsingi huwa yanawekewa vikwazo kwa kufanya kazi na mashirika mengine yaliyoorodheshwa. Hii inaweza kuonekana kama mzunguko; hta hivyo, inaonyesha kuwa mtandao wa mashirika ambao umebuniwa na Korea Kaskazini. Kivingine, kwa kuzingatia asili ya uhusiano wa karibu baina ya mashirika, kutekeleza vikwazo kisheria kwenye shirika moja au zaidi ina uwezekano mkubwa wa kuwa na athari kwa mashirika kdhaa.

   Kwa ajili watu binafsi wanaonekana kutekeleza biasharsa ya fedha nchini Uchina na biashara na ufadhili wa shughuli za usambazaji na silaha kwenye Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati, mashirika wanayofanyia kazi yanauwezekano mkubwa wa kufuata mienendo kama hii. Kama ilivyotajwa hapo juu, nchi wanachama wanafaa kuzingatia kuteua rasilimali zao vilivyo.

Kwa kuszingatia mwingiliano wa karibu baina ya mashirika ya Korea Kaskazini, kushinikiza benki na mashirika ya biashara kwa kutilia nguvu vikwazo vya Umoja wa Mataifa kunaweza kuwa muhimu sana ili kukatiza mitandao ya fedha na biashara ya Korea Kaskazini.

5. Banki au kampuni kadhaa za biashara zilizuiwa na SWIFT, ingawa chache ziliamua kujitoa pindi zilipowekewa vikwazo. Kwa ajili SWIFT ni huduma pekee ya kutuma ujumbe kimtaifa baina ya benki, huduma zingine za kutuma ujumbe wa fedha zinafaa kufutiliwa ili kuangalia kama mashirika yaliyokuwa kwenye SWIFT yamehama ili kurahisisha ukiukaji w vikwazo vya fedha kwa kutumia huduma hizi zingine.

Mawakala mengine baina ya benki yayotoa chaguo mbadala lisilo SWIFT yanafaa kufuatiliwa ili kugundua shughuli za mashirika yaliyoorodheshwa.

6. Mashirika yanayojihusisha kwenye ukiukaji wa marufuku ya bidhaa kwa kutumia vyombo vya baharini yanafanana sana, yaani, yote ni kampuni za usafirishaji za Korea Kaskazini. Licha ya hayo, mashirika mengi yanaweza kubadilisha au kujaribu kuficha majina ya vyombo vya usafirishaji baharini. Yale yanayoonekana kuwa sawia miongoni mwa vyombo hivi vya usafiri ni kuwa vina bendera ya Korea Kaskazini, lakini mra nyingine yana bendera za nchi zingine ambazo huenda zisidadisi maombi ya bendera zao, kama vile Panama na Siera Leoni. Wakiukaji hawa wa vikwazo pia wanaonekana kuwa mara nyingi wanabebea petroli/mafuta au makaa mawe na mara nyingi wanaashiria vituo vyao vya safari ni Vietinamu au Urusi, inagawa wanaweza wasifike kwenye vituo hivi.

Nchi wanachama zinafaa kufuatilia kampuni za usafirishaji za Korea Kaskzini zinazofanya shughuli zao hasa kwa kutumia vyombo vya usafiri vyenye bendera ya Korea Kaskazini, na kimahususi kuwauliza maswali waendeshaji vyombo kuhusu ubadilishaji wowote wa hivi karibuni, bila kujali maeneo wanayoendesha vyombo hivyo.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

7. Mashirika yanayofanya biashara au yanayorahisisha bishara ya bidhaa zilizowekewa marufuku (k.v., bidhaa zenye matumizi mawili, silaha za maangamizi makubwa, silaha) pia yanaonekana kuwa yanafanya mfululizo wa ukiukaji mwingine Kuna uwezekano mkubwa kuwa mataifa yanayofuatilia mashirika ambayo haswa yameorodheshwa kwa ajili ya ukiukaji wa marufuku pia huenda yakaweza kuzingatia au kufuatilia ukiukaji mwingine.

Mashirika yanayohusika sana kwenye uundaji wa Silaha za Maangamizi Makubwa mara nyingi huwa ni mawakala ya serikali ya Korea Kaskazini tu. Mataifa yanayotaka kutekeleza kisheria vikwazo kwa mashirika haya huenda yakanufaika kw kufuatilia mwendo na shughuli za wawakilishi wa serikali wa mashirika haya yaliyoorodheshwa, haswa wale wanaosafiri kama wanadiplomasia.

Kwa jumla, inaonekana kuwa kuna sifa kadhaa za pamoja za watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa ambazo zinaweza kuwa muhimu kwa mataifa kuzifahamu ili kusaidia juhudi zao za kutekeleza sheria za vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Licha ya hayo, ni muhimu kudokeza kuwa sifa hizi zinategemea ripoti za Jopo la Wataalamu na ithibati zingine zinazounga mkono, na kwa hivyo zinaweza kuwa na upungufu wowote uliokuwepo kwenye maelezo ya awali. Kwa mfano, aina zingine za ukiukaji huenda zikawa zinafanyika, lakini Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa huenda likawa bado halijtambua au kuripoti kuhusu masuala haya au masuala mengine. Kwa hivyo, mataifa yanaweza kutumia maelezo haya hapo juu kama miongozo ya sifa za pamoja za wakiukaji lakini yanafaa kuzingati ukiukaji mwingine unaowezekana kuwa unatokea.

Wakati wa kufuatilia mashirika yaliyoorodheshwa kwa ajili ya ukiukaji wa marufuku, tafuta shughuli zingine zinazofanywa na mashirika haya (k.v., miamala ya fedha, shughuli na mashirika mengine yaliyoorodheshwa, kutuma wawakilishi hadi mataifa mengine, n.k.,), kwa ajili inaonekana kuwa shughuli moja itakuwa ina uhusiano na shughuli zingine zinazokiuka vikwazo vya Umoja wa Mataifa.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Nyongeza

Watu Binafsi na Mashirika ya Korea Kaskazini Yanazungumziwa kwa Ufupi

#	Mtu Binafsi	Uhusiano	Uraia	Tarehe ya Kuorodhesh wa
10	Yo'N Cho'Ng Nam	Mwakilishi Mkuu wa KOMID	Korea Kaskazini	2013-03-07
11	Ko Ch'o'l-Chae	Naibu wa Mwakilishi Mkuu wa KOMID	Korea Kaskazini	2013-03-07
16	Jang Bom So	Mwakilishi wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon nchini Siria	Korea Kaskazini	3/2/2016
17	Jang Yong Son	Mwakilishi wa KOMID nchini Irani	Korea Kaskazini	3/2/2016
18	Jon Myong Guk	Mwakilishi wa ng'ambo wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon	Korea Kaskazini	3/2/2016
19	Kang Mun Kil	Mwakilishi wa ng'ambo wa Shirika la Biashara la Namchongang	Korea Kaskazini	3/2/2016
20	Kang Ryong	Mwakilishi wa KOMID nchini Siria	Korea Kaskazini	3/2/2016
22	Kim Kyu	Afisa wa Masuala ya Nje wa KOMID	Korea Kaskazini	3/2/2016
24	Kim Yong Chol	Mwakilishi wa KOMID nchini Irani	Korea Kaskazini	3/2/2016
25	Ko Tae Hun	Mwakilishi wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon	Korea Kaskazini	3/2/2016
27	Ryu Jin	Mwakilishi wa KOMID nchini Siria	Korea Kaskazini	3/2/2016
30	Kim Song Chol	Afisa wa KOMID	Korea Kaskazini	11/30/2016

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

#	Mtu Binafsi	Uhusiano	Uraia	Tarehe ya Kuorodhesh wa
31	Son Jong Hyok	Afisa wa KOMID	Korea Kaskazini	11/30/2016
33	Ri Won Ho	Afisa wa Wizara ya Usalama wa Nchi ya Korea Kaskazini nchini Siria anayesaidia KOMID.	Korea Kaskazini	11/30/2016
34	Jo Yong Chol	Afisa wa Wizara ya Usalama wa Nchi ya Korea Kaskazini nchini Siria anayesaidia KOMID	Korea Kaskazini	11/30/2016
36	Kim Sok Chol	Aliyekuwa Balozi huko Burma, Msaidizi wa KOMID	Korea Kaskazini	11/30/2016
51	Ri Jae Il	Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Poroji na Uchozezi ya Chama cha Wafanyakazi cha Korea	Korea Kaskazini	2017-06-02
56	Jang Song Chol	Mwakilishi wa ng'ambo wa KOMID	Korea Kaskazini	8/5/2017
57	Jang Sung Nam	Shirika la Biashara la Tangun nchini Uchina	Korea Kaskazini	8/5/2017
59	Kang Chol Su	Mwakilishi wa Shirika la Jumla la Ryonbong nchini Uchina	Korea Kaskazini	8/5/2017
62	Pak Il Kyu	Mwakilishi wa Shirika la Jumla la Ryonbong nchini Uchina	Korea Kaskazini	8/5/2017
64	Ch'oe S'ok-Min	Mwakilishi wa Benki ya Biashara ya Nje nchini Uchina.	Korea Kaskazini	2013-12-22
68	Kim Tong Chol	Mwakilishi wa Benki ya Biashara ya Nje huko Shenyang, Uchina	Korea Kaskazini	2017-12-22
70	Ku Ja Hyong	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya Biashara ya Nje	Korea Kaskazini	2017-12-22
72	Pae Won Uk	Mwakilishi wa Benki ya Daesong huko Beijing, Uchina	Korea Kaskazini	2017-12-22
74	Ri Chun Hwan	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya Biashara ya Nje	Korea Kaskazini	2017-12-22
75	Ri Chun Song	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya Biashara ya Nje	Korea Kaskazini	2017-12-22
77	Ri Song Hyok	Mwakilishi wa Kampuni ya Kuendeleza Mikopo ya Koryo na Benki ya Koryo nchini Uchina	Korea Kaskazini	2017-12-22

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

#	Mtu Binafsi	Uhusiano	Uraia	Tarehe ya Kuorodheshwa
80	Tsang Yung Yuan	Aliratibu uuzaji nje wa makaa ya mawe ya Korea Kaskazini na dalali wa Korea Kaskazini anayefanya shughuli kwenye nchi nyingine, shughuli zingine za kukwepa vikwazo	Haihusiki	2018-03-30

#	Shirika	Uhusiano (mmiliki, kampuni ifichayo, mshiriki, inamilikiwa/kuendeshwa na, n.k.)	Tarehe ya Kuorodheshwa
1	Shirika la Biashara za Kuendeleza Uchimbaji Madini la Korea (KOMID)	Kamati ya Pili ya Uchumi	4/24/2009
4	Kampuni ya Biashara ya Namchongang	Ofisi ya Kuu ya Nishati ya Nyuklia (GBAE)	7/16/2009
7	Ofisi ya Kuu ya Nishati ya Nyuklia (GBAE)	Serikali, Kampuni ya Biashara ya Korea Kumsan, Kampuni ya Biashara ya Namchongang	7/16/2009
10	Shirika Husiani la Green Pine	Ofisi ya Jumla ya Upelelezi	5/2/2012
12	Kamati ya Korea ya Teknolojia ya Anga (KCST)	Ofisi ya Taifa ya Uendelezaji wa Anga, Usimamizi wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Vyombo vya Anga	1/22/2013
14	Kampuni ya Biashara ya Korea Kumryong	KOMID	1/22/2013
16	Shirika la Mradi wa Pamoja la Mashine la Korea Ryonha	Shirika la Jumla la Korea Ryonbong	1/22/2013
17	Shirika la Kimataifa la Leader (Hong Kong)	KOMID	1/22/2013
18	Chuo cha Pili cha Sayansi	Kamati ya Pili ya Uchumi wa Kitaifa, Shirika la Biashara la Tangun	2013-03-07
21	Chuo cha Sayansi cha Ulinzi wa Nchi (ANDS)	Chuo cha Pili cha Sayansi Asilia	3/2/2016
23	Banki ya Mkopo ya Daedong	Banki ya Korea Daesong inayomilikiwa na Bw. Li Zhengang (Uchina)	3/2/2016
27	Wizara ya Sekta ya Nishati ya Nyuklia (MAEI)		3/2/2016

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

#	Shirika	Uhusiano (mmiliki, kampuni ifichayo, mshiriki, inamilikiwa/kuendeshwa na, n.k.)	Tarehe ya Kuorodhesh wa
28	Idara ya Sekta ya Silaha (MID)	Kamati Kuu ya Kijeshi ya Chama cha Wafanyakazi wa Korea na Ofisi ya Sera za Utendaji	3/2/2016
29	Usimamizi wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Vyombo vya Anga	Kamati ya Korea ya Teknolojia ya Anga, Kituo cha Jumla cha Kudhibiti na Kuamrisha Satalaiti	3/2/2016
33	Benki ya Maendeleo ya Muungano ya Korea	Ofisi ya Jumla ya Upelelezi	11/30/2016
35	Benki ya Korea Daesong	Ofisi ya 39 ya Chama cha Wafanyakazi cha Korea	11/30/2016
39	Kampuni ya Kimtaifa ya Korea ya Mradi wa Pamoja wa Kemikali (KICJVC)	Shirika la Jumla la Korea Ryonbong	11/30/2016
44	Shirika la Biashara la Korea Kumsan	GBAE	2017-06-02
45	Benki ya Koryo	Ofisi ya 38 na Ofisi ya 39 ya Chama cha Wafanyakazi cha Korea, Kundi la Uchumi la Korea Myohyang, Benki ya Kimataifa ya Koryo	2017-06-02
46	Kikosi Muhimu cha Roketi cha Jeshi la Watu wa Korea	Jeshi la Watu wa Korea	2017-06-02
47	Benki ya Biashara ya Nje	Inamilikiwa na serikali	8/5/2017
49	Benki ya Kuendeleza Mikopo ya Koryo	Ofisi ya 38 na Ofisi ya 39 ya Chama cha Wafanyakazi cha Korea, Benki ya Imani Ulimwenguni ya Koryo, Benki ya ya Kimataifa ya Mikopo ya Koryo	8/5/2017
55	Kampuni ya Usafirishaji na Teknolojia ya Chang An	Mmiliki aliyesajiliwa, meneja wa meli, , na meneja wa biashara wa HUA FU yenye bendera ya Panama	2018-03-30
56	Kampuni ya Usafirishaji ya Chonmyong	Mmiliki aliyesajiliwa wa CHON MYONG 1 yenye bendera ya Korea Kaskazini	2018-03-30
57	First Oil JV Co Ltd	Mmiliki wa tanka la Korea Kaskazini la PAEK MA	2018-03-30
58	Kampuni ya Usafirishaji ya Hapjanggang	Mmiliki aliyesajiliwa na tanka la Korea Kaskazini la NAM SAN 8	2018-03-30
59	Huaxin Shipping Hongkong Ltd	Meneja wa biashara na meli wa ASIA BRIDGE 1 inayomilikiwa na Hong Kong	2018-03-30

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

#	Shirika	Uhusiano (mmiliki, kampuni ifichayo, mshiriki, inamilikiwa/kuendeshwa na, n.k.)	Tarehe ya Kuorodhesh wa
60	Kingly Won International Co., Ltd	Tsang Yung Yuan (pia anajulikana kama Neil Tsang)	2018-03-30
61	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Achim	Mmiliki aliyesajiliwa wa CHON MA SAN yenye bendera ya Korea Kaskazini	2018-03-30
62	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Ansan	Mmiliki aliyesajiliwa wa tanka la Korea Kaskazini la AN SAN 1	2018-03-30
63	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Myongdok	Mmiliki aliyesajiliwa wa YU HYONG 5.	2018-03-30
64	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Samjong	Mmiliki aliyesajiliwa wa matanka ya Korea Kaskazini ya SAM JONG 1 na SAM JONG 2	2018-03-30
65	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Samma	Mmiliki wa SAM MA 2 yenye bendera ya Korea Kaskazini	2018-03-30
66	Korea Yujong Shipping Co Ltd	Mmiliki aliyesajiliwa wa tanka la Korea Kaskazini la YU JONG 2	2018-03-30
67	Kampuni ya Koti	Meneja wa meli na meneja wa biashara wa KOTI yenye bendera ya Panama	2018-03-30
68	Kampuni ya Usafirishaji ya Myohyang	Meneja wa meli wa tanka la YU SON la Korea Kaskazini	2018-03-30
69	Kampuni ya Usafirishaji ya Paekma	Mmiliki aliyesajiliwa wa tanka la Korea Kaskazini la PAEK MA	2018-03-30
70	Kampuni ya Usafirishaji Baharini ya Phyongchon	Mmiliki aliyesajiliwa wa tanka la Korea Kaskazini la JI SONG 6	2018-03-30
71	Shirika la Kundi la Pro-Gain	Kampuni inayomilikiwa na kuendeshwa na Tsang Yung Yuan (mtu #80)	2018-03-30
72	Shanghai Dongfeng Shipping Co Ltd	Mmiliki aliyesajiliwa, msimamizi wa biashara na meli wa DONG FENG 6	2018-03-30
73	Kampuni ya Usafirishaji Kimataifa ya Shen Zhong	Meneja wa biashara na meli wa HAO FAN 2 na HAO FAN 6 zenye bendera ya St Kitts-Nevis	2018-03-30

#	Shirika	Uhusiano (mmiliki, kampuni ifichayo, mshiriki, inamilikiwa/kuendeshwa na, n.k.)	Tarehe ya Kuorodheshwa
74	Kampuni ya Kusafirisha Mizigo Ulimwenguni ya Weihai	Meneja wa biashara na meli ni XIN GUANG HAI	2018-03-30
75	Yuk Tung Energy Pte Ltd	Msimamizi wa biashara na meli wa YUK TUNG	2018-03-30

Shawna Meister - Mchangia Mkuu wa CCSI

Mchambuzi wa sera na utafiti, Shawna Meister amefanya kazi na CCSI tangu ilipanzishwa kwenye miradi anuwai kwa miaka minane iliyopita. Historia yake inajumuisha kuchambua kazi ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa kwenye juhudi za jumla za kusuluhisha vita, vita vya wenyewe kwa wenyewe barani Afrika na kwenye Mashariki ya Kati, changamoto za kutekeleza sheria za vikwazo vya kupinga usambazaji. Hivi karibuni, kama sehemu ya jitihada ya utafiti wa kuainisha ya CCSI, Shawna ameongoza uchambuzi wa sifa na shughuli za watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa ili kutambua ruwaza na uhusiano ndani ya na kwenye mifumo ya vikwazo. Ameandika machapisho kadhaa yakiwemo kuandika ripoti za kiufundi na kichambuzi, uchunguzi wa kifani, makala ya majarida, na amechangia kwenye miongozo ya kupinga usambazaji na vitavu vyote ambavyo vimechapishwa na CCSI. Uhodari wa Shawna unajumuisha usimamizi wa miradi ya utafiti yenye daraja anuwai na kugeuza uchambuzi na maelezo tata yawe bidhaa zinazoweza kutumika kama vile miongozo ya mafunzo, miongozo ya kielimu, rasilimali na vifaa vya umma, na tovuti.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com